**Kila mtu ana malaika (05) - Maana ya kuwa na virusi vya ukimwi**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika:**

Anita
Mjomba Billy (kwenye simu)
Djamila
Mamake Djamila
Mjomba Imrat
Tom
Annie
Angela
Spike
Pinto (kwenye simu)

**Utangulizi:**

Karibu tena kwenye kipindi cha sikiliza ujifunze ambapo tunaingie kwenye kisa kingine cha mfululizo wa mchezo wa kuigiza Malaika wa kila mtu,amchezo ambao unawaangazia vijana wanaojihatarisha,lakini pia watu wazima ambao tabia zao za kujihatarisha zinawatia vijana katika hatari ya maisha. Angela msichana mwenye umri wa miaka 17 amepata mamba na amepimwa virusi vya HIV lakini anatafuta majibu juu ya virusi hivi vya HIV vinamaanisha nini.Mmake amepania kumfukuza nyumbani ili aende akaishi na kijana aliyempa uja uzito,Pinto ambaye ana umri wa miaka 19. Katika kisa cha leo Rafiki yake Angela,Djamila anajaribu kuzungumza na mamake kuhusu kupima HIV.Lakini mjomba wake Imrat anawatembelea.Je anataka nini? Na je kwanini Tom anaonyesha kuwa na shauku na Annie? Ungana nasi ili upate majibu yote hayo katika sehemu ya tano ya mchezo "Malaika wa kila mtu".

**SURA YA KWANZA: JIKONI**

| | |
|---|---|
| SFX | Simu ya mkono inalia. |
| ANITA: | Hallo! |
| BILLY: | (akizungumza kwenye simu) Anita. |
| ANITA: | Ndio Billy sema |
| BILLY: | Sikiliza dada nimezungumza na Pinto na familia yake |
| ANITA: | Enhe? Imekuwaje |
| BILLY: | Ahhh - walishangaa bila shaka, kwa kweli wote hawakuamini macho yao. |
| ANITA: | Kushangaa hakutamsaidia yoyote kwa sasa kakangu, wewe muache Angela aende huko kulikokuwa na Party na vinywaji kila aina na wanaume mimi sitaki kujua. |

| | |
|---|---|
| BILLY: | Ehh Dada muogope Mungu wewe ndugu yangu, Angela ana umri wa miaka 17 tu, huwezi kumfunga kamba kiasi hiki. Layla na Mo ni mabinti wazuri, na ingawa hivyo ni wadogo na wanapenda kula raha. Lakini hawakupata mamba. |
| ANITA: | Oooh! Unasemaje, ni kwa sababu yao ndo mwanangu… |
| BILLY: | (Anamkatiza) Hivyo ndivyo anavyosema mwanao Angela kwamba hilo lilikuwa kosa lao kwa kuwa walikwenda nyumbani kwa huyo kijana? Sikiliza dada hebu tuyazungumze kwa makini. Yeye alilala na Pinto wenzake waliondoka! |
| ANITA: | Angalau basi wangemlinda |
| BILLY: | Lakini yeye ni mkubwa kuwaliko wenzake. Angejitunza mwenyewe. Wanangu wanajua barabara kukataa mambo ya kipuuzi aina hiyo, sasa Angela hajui. Sikiliza siwezi kupoteza muda wangu. Nilipiga tu kukueleza kwamba nilizungumza na Pinto. Anajua, amesema atampigia simu Angela usiku. |
| SFX | MUZIKI WA KUFUNGA |

**SURA YA PILI: KWENYE BUSTANI**

| | |
|---|---|
| SFX | SAUTI ZA NDEGE/MITI |
| DJAMILA: | Mmm mama hayo ndo maua unayoyapenda sana |
| MAMA: | Naam nayapenda mno mwanangu maua haya. |
| DJAMILA: | Yanaitwaje? |
| MAMA: | Petunias,yana harufu  nzuri sana,lakini inabidi uyakate matawi kidogo halafu yataanza tena kuchanua maua. (Kimya kidogo) Angela jana alikaa muda mrefu kidogo. Kulikuwa na matatizo yoyote? |
| DJAMILA: | Ndio mama ah lakini yuko sawa hana neno. (Kimya) Eh mama umeyaona mabango ya matangazo yaliwekwa mjini, umeyaona? |
| MAMA: | Sijayaona, yapi hasa unayoyazungumzia wewe? |
| DJAMILA: | Ummm sawa basi kuna mabongo makubwa yamewekwa katika kona ya mzunguko wa barabara ile ya kuingilia shule kwetu. |
| MAMA: | (Akisita sita) Oh yale ndio nimeyaona hapa nyumbani. Masuala namna ile sitaki kuyasikia kabisa wala hatuyajadili. Kwa nini unaulizia Djamila? |
| DJAMILA: | Ahh wajua nini mama nilikuwa najaribu tu kutaka kujua inamaanisha nini? |

| | |
|---|---|
| MAMA: | Mwanangu we mwangangu, kwa nini unauliza vitu kama hivyo? Hatuna haja ya kuonja. Tunakuwa waaminifu kwenye ndoa kama unavyofahamu, hakuna msichana anyeruhusiwa kufanya mapenzi nje ya ndoa. Haya mambo yote kuhusu HIV hayatuhusu sisi wala wewe. Sasa unachotaka kujua nini hasa?Au inahusiana cho chote na rafiki yako Angela? Ennhhh? |
| DJAMILA: | Sio hivyo mama! Hapana, ni kwa sababu nimeona tu Kwenye mabango yale kumeandikwa nenda ukapime, kwa hiyo nilifikiri unajua pengine ninatakiwa kufanya hivyo. |
| MAMA: | Akicheka. Hapana hapana mwanangu, wewe tunakulinda na - lo, tazama mjomba wako Imrat yule anakuja. |
| SFX | Mlio wa gari linalokaribia, mlango wa gari unafunguliwa - unafungwa. Anatembea. |
| IMRAT: | (Kando ya mic) habari gani dadangu mzuri. (kwenye mic) Na Djamila hujambo na wewe, huna neno? (anambusu) |
| DJAMILA: | (akiona aibu) Sijambo mjomba. |
| IMRAT: | Kitu gani tena? Kwani siruhusiwi kumbusu mpwa wangu shavuni? Ala vipi, hebu njoo. (Anambusu) |
| DJAMILA: | (Akilalamika) hebu mjomba, tafadhali… |
| MAMA: | We Djamila hebu wacha upuuzi wako… Ah kweli! (Anambusu) Imrat nafurahi sana kukuona, haya pita ndani basi. |
| SFX | SAUTI ZA WATU KUPITAPITA.MLANGO UNAFUNGWA. |
| MAMA: | Haya hebu kaeni nyote wawili. Djamila hebu zungumza na mjomba wako, mie naandaa chai. |
| DJAMILA: | (Adakia) Hapana mama, eh nimekumbuka kitu, inabidi niende nikafuate kitu jikoni, kwanza hiyo chai nitaiandaa mimi Ma Usijisumbue… (Kando ya mic) sitachukua muda mrefu… |
| MAMA: | (Anacheka) Mtoto huyu! Basi tena… |
| IMRAT: | Namsikitikia mwanao, kila panapokuwa na mwanamume karibu anaona aibu tuu. |
| SFX | MUZIKI WA KUMALIZIA |

**SURA YA TATU: DUKANI**

| | |
|---|---|
| SFX | Sauti za watu pita pita na makelele ya dukani |
| ANNIE: | Asante Spike mmmh hizi nzuri kweli kweli. |

| | |
|---|---|
| SPIKE: | (Kwa sauti ya kutongoza) Nataka nikuone ukiwa umezivaa leo usiku, ili… wajua tena… nizivue… |
| SFX | SAUTI YA MTU AKITEMBEA - MLANGO UKO WAZI |
| ANNIE: | Tutaonana baadae kwenye kituo cha texi Spike - sasa hivi nataka kwenda kununua mkate. |
| SPIKE: | (Kando ya Mic) Usichelewe basi |
| TOM: | Ooh. Vipi, Annie! |
| ANNIE: | (Kwa aibu) Tom! |
| TOM: | Mambo vipi? |
| ANNIE: | Ha, hakuna |
| TOM: | Hereni nzuri hizi! |
| ANNIE: | Hereni? Ah oh asante. |
| TOM: | Yule aloondoka ndo yule dereva wa taxi mwenyewe nini Annie, Mbona yuko ovyo ovyo kweli. |
| ANNIE: | Mm wasemaje? Nini ni mzuri |
| TOM: | Vipi Annie, mkono wako mbona kidogo umekwaruzika, ulifanyika nini? |
| ANNIE: | Mkono wangu? Ah, hii alama! (acheka kwa kejeli) Umekwaruzika zaidi kuliko unavyoonekana hapa. Ouch! Usiniguse bwana naumia. |
| TOM: | Pole! |
| ANNIE: | Nilijigonga na mlango tu, hakuna cha ziada, sikiliza Tom, wacha nende zangu. Jet ananisubiri. |
| TOM: | Jet? Yule mzee mwenye gari ya kifahari? Na Spike ndo nani? |
| ANNIE: | Hebu sikiliza wewe, hakuna la kukuhusu hapo. Fuata shughuli zako, achana na mambo yangu. |
| TOM: | Si nilifikiri ulitaka kwenda kunua mkate. |
| ANNIE: | Mkate? Ah achana nao mkate wa nini, shughuli hiyo itafanywa wakati mwingine. Bye Tom. |
| TOM : | (Kwa huzuni) Pole sana Annie - lakini sipendi wanaume wanaowaumiza wanawake. Ukitaka nifanye chochote kile nitafanya -wajua ninachomaanisha. Unajua kwamba naweza kufanya lolote kwa ajili yako, nambari yangu unayo? Basi wewe nipigie, kama rafiki. |
| SFX | Muziki unapotea, sauti zinapotea. |

**SURA YA NNE: SEBULENI**

| | |
|---|---|
| ANITA: | Angela nilizungumza na mjombako Billy asubuhi. |
| ANGELA: | Mama tafadhali usianzishe tena mjadala huo. Mimi nataka kuishi hapa. |
| ANITA: | Mpuuzi sana mtoto wewe yaani unafikiri utaendelea |

| | |
|---|---|
| | kuishi na mimi hapa kama ambaye hakuna kitu kibaya kilichotendeka? Wajidanganya, tena sahau kabisa. Yule mvulana wako alokutwika huo mzigo ndo baba mtoto wako, kwa hivyo lazima utakwenda huko huko. |
| ANGELA: | (Ashusha pumzi) Umezungumza na Pinto? |
| ANITA: | Hapana, lakini mjombao Billy amezungumza nae. Na huyo Pinto zako atakupigia simu usiku. |
| ANGELA: | Eti atanipigia simu? Sasa ntazungumza nae nini? Ntasema nini? |
| ANGELA: | Utajua cha kuzungumza, si utamwambia unakwenda kwake na yeye aseme tu lini uende. Mimi ntakupeleka binafsi hukai hapa nakwambia, mimi ni mamako na siwezi kukuruhusu ukae hapa na mtumbo wako wa mamba kila mmoja akuone hapa mtaani una mamba, kuniaibisha tu usokuwa na adabu. Mimi sio wale wazazi wanafumbia macho uovu kama huu kwa kutaka kufaidika, sio mimi umesikia. Katika mila zetu unapasa kwenda huko huko kwa alokujaza hiyo mimba. |
| ANGELA: | (Analia) Marafiki zangu wote wako hapa mama, shule iko hapa Ma, na pia naingia kwenye mtihani wa mwisho wa kidato cha nne mwaka huu Ma. |
| ANITA: | (acheka kwa kejeli) alaaa ungekuwa umeyafikiria hayo kabla ya kulewa na kulala na mtu usomjua kichwa wala miguu. |
| ANGELA: | Mama ilikuwa ni Party tu, sikujua kama yote yangetokea, sikujua kama… ah sasa nieleze vipi mimi. Sikujua mama, nisamehe, tafadhali mama nisamehe. Mungu wangu natamani hata ningejiua nikaondoka duniani. |
| ANITA: | Na huyo mtoto pia! Ufanye dhambi mara mbili. Huna maadili wewe? Kwa nini unasema maneno kamahayo, huyo Pinto si ndo babake. Basi yeye na familia yake lazima wachukue majukumu. |
| ANGELA: | Mama tafadhali usinifanyie hivi, tafadhali usinifukuze. |
| ANITA: | Nakwambia hivi, kama hujasikia vizuri… nyumba hii haikuhusu tena. Umebakisha miezi miwili tu ujifungue. Sasa wataka kunambia baada ya kuzaa utarudi shule? Niondokee mie! Tena hilo sahau! Utakwenda kwa Pinto wako wataka hutaki! Tena jumapili kwa hiyo anza kufunga virago vyako. Mtoto umekosa adabu kweli kweli, umenitia aibu kubwa, sasa utavuna ulichokipanda. |
| SFX | MUZIKI WA KUMALIZIA |

## SURA YA TANO: USIKU NDANI

| | |
|---|---|
| SFX | Sauti za usiku, sauti ya simu |
| PINTO: | (Kwenye simu) Hallo Angela? |
| ANGELA: | Naam ni mimi. |
| PINTO: | (Kwa uoga) Vipi, habari gani, mimi Pinto hapa. Nimesikia kuhusu... aah, mjombako Billy amenambia. Sasa sikiliza Angela, nnachoweza kusema ni kwamba nakuomba msamaha sana. |
| ANGELA: | Mamangu amenikasirikia kweli, ananifukuza nyumbani. |
| PINTO: | Najua,naelewa Angela, na mtoto? Lazima utakuwa unakaribia kujifungua. |
| ANGELA: | Ndio, nimebakisha kama wiki 8 hadi 10. Lakini Pinto… kuna mambo mengine lazima tuyazungumze. |
| PINTO: | (Amkatiza) Sio kwenye simu lakini, tafadhali Angela... (kimya) |
| ANGELA: | (kwa unyonge) Hakuna tatizo. |
| PINTO: | Sasa… aah unaweza kuja kuishi huku, je uko tayari kuja Jumapili ijayo? Njoo ukishatoka kanisani. Ukija hesabu nyumba 15 kutoka kwa mjomba wako, upande wa chini, karibu na duka. |
| ANGELA: | Mamangu anataka kunileta mwenyewe. Na hatakufurahikia. |
| PINTO: | (Acheka) Asante kwa kunitahadharisha mapema, sikiza Angela, hii sio hali nzuri lakini tutajaribu tu, unasikia. Usitie shaka. |
| ANGELA: | Hatuna la kufanya lazima tuyakubali maisha yetu. Haya Pinto basi usiku mwema. Tuonane jumapili. |

## Hitimisho:

Malaika wa kila mtu ni mchezo uliotungwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba. Mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha sikiliza Ujifunze kwa leo. Jiunge nasi tena katika sehemu nyingine ya mchezo huo ambapo hatimae Angela anatafuta ushauri wa kisawa sawa na baba sukari wa Annie nae anaamka asubuhi na kujikuta na upele kwenye sehemu zake nyeti. Usikose kujiunga nasi tena.

Kumbuka ukitaka kuusikiliza tena mchezo huu au kuwaambia marafiki Juu ya mchezo huu unaweza kutembelea tuvuti yetu kwa anuani ya www.dw-world.de/lbe.

Kwa heri.